

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**WIZARA YA MAJI**

Simu: +255 (0) 26 2322602  
Tovuti: [www.maji.go.tz](http://www.maji.go.tz)  
Barua pepe: [ps@maji.go.tz](mailto:ps@maji.go.tz)



Mji wa Serikali,  
Mtaa wa Maji,  
S. L. P. 456,  
**DODOMA.**

Dodoma: 03 Oktoba, 2019

**TAARIFA KWA UMMA**

**BODI YA WAKURUGENZI YA MAMLAKA YA MAJI MOROGORO YAVUNJWA**

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) imevunjwa. Hatua hiyo imechukuliwa na Waziri wa Maji Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb) kuanzia tarehe 02 Oktoba, 2019.

Taarifa ya Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Kitila Mkumbo imeainisha kuwa kuvunjwa kwa bodi hiyo ni kwa mamlaka aliyo nayo Waziri wa Maji kwa mujibu wa kifungu Namba 14 cha Jedwali la kwanza la Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Namba 5 ya Mwaka 2019, kikisomwa pamoja na Kanuni Na. 14 ya Kanuni za Usambazaji wa Maji (Tangazo la Serikali Na. 90 la tarehe 26/04/2019).

Taarifa hiyo imefafanua kuwa bodi ya MORUWASA imevunjwa kwa kushindwa kutekeleza majukumu yake ya kuisimamia mamlaka ya maji hivyo kuathiri utoaji wa huduma za majisafi na usafi wa mazingira katika manipaa ya Morogoro.

Aidha, wakati huo huo Waziri wa Maji Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb) ametaka kuanza kwa utaratibu utakaowezesha kuundwa kwa bodi mpya.

**Kitengo cha Mawasiliano**